MAELEZO YA MWELEKEO WA HATUA ZA UANZISHWAJI WA

USIMAMIZI SHIRIKISHI WA MISITU

Hatua

1: Uhamasishaji

2: Kuunda Kamati ya Mali Asili ya Kijiji

3: Kuchambua matatizo yatokanayo na misitu

4: Kupanga matumizi bora ya ardhi ya kijiji

5: Kukubaliana kuweka mpaka wa kijiji

6: Kupata mamlaka ya kumiliki ardhi ya kijiji

7: Kuweka mipaka ya kijiji

8: Tathmini Shirikishi ya Mazao ya Misitu

9: Kuandaa mpango wausimamizi wa eneo la Msitu wa Kijiji

10: Kutunga sheria ndogo za kusimamia na kuendeleza Msitu wa Kijiji

11: Kutangazwa kwa eneo la Msitu wa Kijiji

12: Utekelezaji wa mpango wa usimamizi wa eneo la msitu

Utangulizi wa
Usimamizi Shirikishi wa Misitu

Mkakati wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu (USM) unaipa jamii sehemu kubwa ya utekelezaji na manufaa; ni mkakati unaolenga katika kuyaweka maeneo mengi ya misitu chini ya usimamizi madhubuti na endelevu. Utaratibu huu unatumika kwenye misitu isiyohifadhiwa ndani ya kijiji au ardhi huria, na Misitu ya Hifadhi (aidha ya Serikali Kuu, Serikali za Mitaa au Serikali za Kijiji). Katika mkakati huu mgawanyo wa majukumu huwekwa bayana.

Mpango huu wa taifa wa USM umeanzishwa kisheria, ambapo umerasimishwa na vyombo vifuatavyo, Sera ya Taifa ya Misitu ya Mwaka 1998, Mpango wa Taifa wa Misitu wa Mwaka 2001, Mwongozo wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu Tanzania wa 2001, Sheria ya Misitu na. 14 ya 2002, na Kanuni za Undeshaji wa Msitu 2004.

Lengo la usimamizi shirikishi wa msitu ni uhifadhi, uvunaji na/au mchanganyiko wa yote. Jamii zinazoishi karibu na misitu zinahusika kwa sehemu kubwa katika utekelezaji. Ili malengo yaliyowekwa ya USM yaweze kufikiwa jamii zinashauriwa kushiriki kikamilifu katika kutekeleza hatua mbalimbali zilizopendekezwa.

Kila jamii ya kijiji itakayoshiriki kusimamia eneo lake la msitu kwa kufuata utaratibu uliopendekezwa watakuwa wamejiongezea kipato kutokana na biashara ya mazao ya misitu na kujikwamua katika mpango wa kupunguza umasikini.

Wataalam wa misitu katika idara ya maliasili Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa wao kama wawezeshaji katika mpango huu wa USM wako tayari kushirikiana na kijiji, kikundi, au mtu mmojammoja katika kutekeleza malengo ya USM.

Hatua zilizopendekezwa

1: Uhamasishaji

Hatua ya mwanzo ya USM ngazi ya kijiji ni kuitisha mikutano ya uhamasishaji. Timu ya wawezeshaji ikishirikiana na jamii hukaa pamoja na kuchambua matatizo yanayohusiana na misitu/mazingira katika kijiji husika na kupanga ufumbuzi kutokana na matatizo hayo.

Chini ya mpango huu wa USM, wanajamii wanayohaki ya kujifunza, pamoja na madaraka ya kushiriki kikamilifu katika kuendeleza mpango huu.

2: Kuunda Kamati ya Mali Asili ya Kijiji

Kamati ya Mali Asili ya Kijiji ni kamati itakayokuwa inasimamia na kuratibu shughuli zote za maliasili kijijini. Kamati hii inatakiwa iwe na wajumbe wasiopungua kumi na mbili na theluthi moja wawe wanawake. Wajumbe hawa huchaguliwa na mkutano mkuu wa kijiji. Sifa au vigezo vya kuchaguliwa kwao ni uaminifu na wenye kujitolea katika kutunza mazingira ya kijiji chao na uzoefu wa kutembea msituni. Ni vizuri wajumbe wengi wa kamati ya maliasili wakawa wanajua kusoma na kuandika na wachache wasiojua kusoma na kuandika wakawepo kwa ajili ya ushauri na kutoa uzoefu wao wa kufahamu mazingira ya msitu.

3: Kuchambua matatizo yatokanayo na misitu

Kazi kubwa ya kamati ya maliasili ya kijiji ni kuangalia matatizo yote yatokanayo na misitu iliyopo kijiji kwao.



Kutambua ardhi za kijiji pamoja na matumizi yake

4: Kupanga matumizi bora ya ardhi ya kijiji

Wanakijiji wanatakiwa kuchora ramani kubwa ya matumizi bora ya ardhi ndani ya kijiji chao, ikionyesha mpaka wa kijiji na mipaka ya matumizi bora ya ardhi ndani ya kijiji ikianisha maeneo kama; makazi, kilimo, misitu, malisho, na shughuli nyingine za maendeleo.

5: Kukubaliana kuweka mpaka wa kijiji

Hatua inayofuata ni kijiji kukubaliana kuwa na mpaka kwa kuvishirikisha vijiji jirani. Kijiji husika kitaitisha mkutano na vijiji jirani ili kukubaliana wapi mpaka utapita na alama zake. Kwa vijiji vinavyotenganishwa na barabara, korongo au mto inakuwa ni rahisi kukubaliana kwa kutumia alama za asili.

6: Kupata mamlaka ya kumiliki ardhi ya kijiji

Muhtasari ulioandaliwa na viongozi wa vijiji upelekwe kwa Afisa Ardhi wa Wilaya, kwa ajili ya kuhalalisha mpaka uliowekwa utambulike kisheria. Kwa utaratibu hakuna uvunaji utakaofanyika ndani ya eneo la kijiji bila idhini ya Serikali ya Kijiji. Kijiji kilichopimwa kinatakiwa kuwa na cheti cha ardhi.

7: Kuweka mipaka ya kijiji

Ili kijiji kiweze kuwa na cheti cha ardhi kinatakiwa kushirikiana na Afisa Ardhi pamoja na Wapimaji wa Ardhi wa Wilaya ili waweze kuweka alama za mipaka zinazokubalika na baadae ni lazima wachore ramani na wapewe nakala ya ramani ya mipaka hiyo.

Mpango wa namna ya utunzaji bora wa misitu

8: Tathmini Shirikishi ya Mazao ya Misitu

Wataalam wa misitu toka wilayani watasaidiana na wajumbe wa kamati ya mali asili ya kijiji kufanya tathmini ya mazao ya misitu ndani ya msitu wao wa kijiji. Watajifunza ni jinsi gani kila kaya inavyotumia mazao yatokanayo na misitu. Vilevile ni vizuri wakajua kila kaya inatumia mazao gani ya misitu na kwa kiasi gani.

Wataalamu kutoka wilayani watashirikiana na Kamati ya Mali Asili, kutambua mahitaji ya mazao ya misitu toka katika msitu wao wa kijiji na kuangalia hali halisi ya misitu, mahitaji mbalimbali ya misitu yaliaopo hivi sasa na mazao yapi ya misitu yangefaa kuvunwa. Kazi hii itachukuwa muda mrefu kwa sababu inahitaji kuchora ramani ya msitu, kutumia muda mwingi kwa kuhesabu na kupima miti hivyo basi itachukuwa muda mrefu kupata tathmini ya mazao ya misitu.

9: Kuandaa mpango wa usimamizi wa eneo la Msitu wa Kijiji

Taarifa zilizokusanywa za msitu zitatumika katika kuandaa mpango kazi wa msitu wa kijiji. Ni muhimu wajumbe wengi kushiriki wakati wa zoezi la tathmini shirikishi ya mazao ya msitu na kuandaa mpango kazi wa msitu wa kijiji, kwa kuwa mpango kazi ni dira/mwongozo utakaotumika katika kutekeleza majukumu yote yanayohusiana na msitu hapo kijijini kwa wakati uliopo na miaka ijayo.

Utaratibu wakukamilisha ili kuwa na eneo la Msitu wa Kijiji

10: Kutunga sheria ndogo za kusimamia na kuendeleza Msitu wa Kijiji

Kipengele kimojawapo katika mpango kazi wa msitu wa kijiji ni kutunga na kupitisha sheria ndogo za Msitu wa Kijiji. Sheria ndogo hutungwa ili kusaidia kusimamia na kuendeleza Msitu wa Kijiji. Kwa kawaida sheria ndogo hupendekezwa na wajumbe wa kamati ya maliasili na kupitishwa na wajumbe wa serikali ya kijiji, mkutano mkuu wa kijiji, na baadaye kupitishwa na kamati ya maendeleo ya kata na Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya.

11: Kutangazwa kwa eneo la Msitu wa Kijiji

Baada ya mpango kazi na sheria ndogo za msitu wa kijiji kupitishwa na ngazi zote kuanzia kijiji hadi Halmashauri ya Wilaya, matangazo huandikwa kuonyesha eneo la msitu wa kijiji lenye ukubwa fulani limetengwa kama eneo la msitu wa jamii wa kijiji husika. Hapo ndipo taratibu za kuvuna na kuboresha msitu hufanywa kutokana na malengo yaliyoainishwa katika mpango kazi. Fedha za makusanyo ya mapato yatokanayo na mazao ya misitu hubaki katika kijiji kama ilivyoainishwa katika mpango kazi wa msitu wa kijiji.

12: Utekelezaji wa mpango wa usimamizi wa eneo la msitu

Hii ni hatua ya mwisho ya utekelezaji wa mpango wa usimamizi wa eneo la msitu, ambao utahusisha kamati ya maliasili na jamii kama itakavyokuwa imeainishwa katika mpango huo.

Kijarida hiki kimeandaliwa na Mradi wa Kuhifadhi Mpingo (MCP) kwa msaada wa Mpango wa Tuzo ya Kuhifadhi Mazingira wa Shirika la Mafuta la BP.